

18 - At-Tafkhiym Na At-Tarqiyq - Kutamka Herufi Kwa Unene Au Wembamba

التَّفْخِيمُ وَالتَّرْقِيقُ

التَّفْخِيمُ At-Tafkhiym - Kufanya Nene Au Nzito (mdomo kujaa)

Maana yake: Kufanya nene au kuitamka kwa uzito.

Katika hukmu ya Tajwiyd ni kuitamka herufi kwa kuifanya nene na nzito nayo hupatikana kwa kupandisha ulimi juu kwenye sakafu ya kinywa hadi kukifanya kinywa kijae inapotamkwa herufi.

التَّرْقِيقُ At-Tarqiyq - Kufanya Nyembamba au Nyepesi

Maana yake: Kufanya nyembamba au nyepesi.

Katika hukmu ya Tajwiyd ni kuitamka herufi kuifanya nyembamba na nyepesi, nayo hupatikana kwa kuteremsha ulimi uwe mbali na sakafu ya kinywa (uwe chini) hadi kukifanya kinywa kisijae.

Tafkhiym na tarqiyq katika herufi za hijaa iyah ziko katika hali tatu:

1. تَفْخِيمٌ دَائِمًا Tafkhiym daima

Ni herufi za الإِسْتِغْلَاءُ (al-isti'laa - kupaa juu) nazo ni; خص ضغط قظ . Uzito wa tafkhiym hauko sawa katika herufi za الإِسْتِغْلَاءُ (al-isti'laa) kwa sababu herufi ظ ص ض ط zina swiffah ya الإِطْبَاق (al-itwbaaq -kufunga) ambazo ulimi unagandamiza sakafu ya kinywa. Hivyo basi huwa ni nzito zaidi kuliko herufi غ ق غ ق ambazo ulimi, sehemu yake ya mbele unalala chini ya kinywa.

Pia herufi za تَفْخِيمٌ (tafkhiym - nzito) hupishana uzito wake kutegemea na daraja ya *i'raab* zake. Kwanza huwa nzito zinapobeba fat-hah na zikafatiwa na أَلِف (alif) kisha fat-hah isiyo na أَلِف (alif), kisha dhwammah, kisha sukuwn na mwisho kasrah.

Inapobeba kasrah	Inapobeba sukuwn	Inapobeba dhwammah	Inapobeba fat-hah
مُبْصِرُونَ	يَسْتَضَعِفُ	الْقُرَّاءُ	الضَّالِّينَ
الْمُسْتَقِيمَ	مَغْفِرَةً	طُوبَى	طَائِفٌ
الْعَظِيمُ	خَلَقْنَاكُمْ	الْخُلَطَاءِ	خَالِدِينَ

2. تَرْقِيقُ دَائِمًا Tarqiyq Daima

Ni herufi zote zilizobakia za اِسْتِفَال (istifaal -kuinamisha) isipokuwa herufi mbili ر na ل. Herufi zilizo na swiffah ya اِسْتِفَال (istifaal) zitamkwe kwa kuteremsha ulimi ili zibakie kuwa ni تَرْقِيقُ (tarqiyq - nyepesi) mifano:

فَأَمَّا مَنْ أَوْقَرَ كَتَبَهُ بِيَمِينِهِ ①

وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ②

إِنَّهُ هُوَ يُبَدِّلُ وَيُعِيدُ ③

3. بَيْنَ التَّفْخِيمِ وَالتَّرْقِيقِ Baina ya Tafkhiym na Tarqiyq

Ni herufi ambazo hutokea zikawa baadhi ya wakati zikawa ni تَفْخِيمُ (tafkhiym - nzito), na wakati mwengine zikawa ni تَرْقِيقُ (tarqiyq - nyepesi) kutegemea na hali inayokutana nazo.

¹Al-Inshiqaaq (84: 7)

²Ash-Shams (91 : 7)

³Al-Buruwj (85: 13)

- i) Alif (ا) ya madd
- ii) Laam (ل) ya Lafdhw Al-Jalaalah (الله)
- iii) Raa (ر)